

4

Bwana Yesu aweza kuokoa na kuhifadhi.

Aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee. Waebrania 7:25.

Yeye aweza kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu. Yuka 24.

Kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa. Waebrania 2:18.

Mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya. 2 Wakorintho 5:17

Kwa Hiyo

Tubu

Mungu... sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Matendo 17:30.

Amini

Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. Matendo 16:31.

Umwungamie Mungu dhambi zako

Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. 1 Yohana 1:9.

Umkiri Kristo mbele za watu

Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. Warumi 10:9, 10.

4

Mambo manne ambayo mwenyezi Mungu ataka uyajue

1

Ataka ujue ya kwamba una haja ya kuokolewa.

kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Warumi 3:23.

Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe. Isaya 53:6.

Watu wanawekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu. Waebrania 9:27.

Mshahara wa dhambi ni mauti. Warumi 6:23.

Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Yohana 3:3.

Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Yohana 3:6.

2

Ataka ujue ya kwamba huwezi kujiokoa.

Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti. Mithali 14:12.

Mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria. Wagalatia 2:16.

Mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Waefeso 2:8, 9.

Yesu alisema, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. Yohana 14:6.

Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. Matendo 4:12.

3

Mungu amekuletea njia ya wokovu.

Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu. 1 Wathesalonike 5:9, 10.

Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16.

Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote. Isaya 53:6.

Kristo aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu. 1 Petro 3:18.

Karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. Warumi 6:23.